# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED GHARIB BILAL, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE HAFLA YA KUWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA VITUO VYA MAPUMZIKO NA VYOO KWA WASAFIRI KATIKA BARABARA KUU NCHINI, IDETERO- MUFINDI MKOANI IRINGA,

**TAREHE 17 OKTOBA 2015**

**Mhe. Dkt. Binilith Mahenge, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira);**

**Mhe. Amina Masenza , Mkuu wa Mkoa wa Iringa;**

**Mh. Balozi wa China nchini Tanzania;**

**Wakuu mbalimbali wa vyombo vya Ulinzi na Usalama mliopo;**

**Viongozi mbalimbali wa Serikali na Vyama vya Siasa mliopo;**

**Ndugu Godfrey Mosha, Mwenyekiti Mtendaji wa Mufindi Enviromental Trust (MUET);**

**Ndugu Wanahabari;**

**Ndugu Wananchi;**

**Wageni Waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana**

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uzima na afya njema nakutuwezesha kukusanyika hapa siku ya leo, kufanya jambo hili muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Nichukue nafasi hii pia kushukuru uongozi mzima wa Mufindi Enviromental Trust ( MUET) kwa kunialika kuwa Mgeni rasmi katika hafla hii ya *Kuweka Jiwe la Msingi Mradi wa Vituo vya Mapumziko na Vyoo kwa Wasafiri katika Barabara Kuu nchini*. Nimepokea mwaliko huu kwa mikono miwili. Asanteni Sana! Nitumie nafasi hii pia kushukuru wananchi na uongozi mzima wa Mkoa wa Iringa, chini yako Mheshimiwa Masenza, kwa moyo wa ukarimu na mapokezi mazuri mliyonipa mimi pamoja na ujumbe wangu. Asanteni Sana!

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana;**

Nimefarijika sana kusikia jitihada mbalimbali zinazofanywa na MUET kwa kushirikiana na wadau wengine katika suala zima la uhifadhi na utunzaji mazingira ya nchi yetu. Shirika hili tangu kuanzishwa kwake, limefanya mambo mengi, ikiwa ni pamoja na; Kuhamasisha upandaji miti kwa watu binafsi, kampuni taasisi za dini na Serikali, Kuboresha vyanzo vya maji; Kutoa elimu ya kuzuia uchomaji misitu na Kutoa elimu juu ya ugonjwa hatari wa Ukimwi. Nazidi kuwatia moyo kuendeleza juhudi hizi njema kwa

nguvu kubwa kwani mazingira ni muhimu sana katika maisha ya kila siku ya viumbe hai wakiwemo binadamu.

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana;**

Ili kujenga nchi yetu ,tunahitaji watu wenye afya bora. Moja ya mambo muhimu katika kuboresha afya za watu wetu ni suala zima la usafi. Hatuwezi kuzungumzia usafi katika mazingira tunayoishi bila kutaja suala la vyoo. Huwezi kujiita msafi au mtu uliyestaarabika kama nyumbani kwako huna choo kizuri na safi. Choo ni usafi namba moja katika mazingira tunayoishi. Hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha anachimba choo na kukitunza katika mazingira ya usafi. Choo ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku, kuwa na choo peke yake haitoshi kama choo hicho hakitunzwi katika mazingira ya usafi.

Nitumie fursa hii kuwapongeza MUET kwa ubunifu wenu wa kuanzisha vituo vya mapumziko na mradi wa kuchimba vyoo katika barabara kuu nchini. Kwa muda mrefu abiria wanaosafiri katika barabara kuu, wamekuwa wakipata tabu pindi wanapohitaji sehemu za faragha za kujisitiri. Jambo hili limefikia katika hatua mbaya hata kukiuka ustaarabu wa kibinadamu kwa kujisadia porini kama wanyama kwa lugha maarufu ya *"kuchimba dawa".* Tabia hii si ya ustaarabu inadhalilisha utu wetu. Karne ya leo si ya kuendelea "*kuchimba dawa."* Hatua ya MUET kubuni jambo hili inastahili pongezi na kuungwa mkono na wadau wote ili kuhakikisha malengo yake yanatimia kwa kujenga

vituo vya mapumziko na vyoo vya wasafiri katika barabara zote nchini.

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana;**

Serikali ya awamu ya nne na zilizotangulia, imefanya jitihada kubwa kuimarisha sekta ya miundombinu ya barabara nchini. Tunapozungumza leo karibu mikoa yote nchini imeunganishwa kwa barabara za lami. Mafanikio haya si ya kubezwa hata kidogo. Hatua ya kubuni mradi huu katika barabara hizi, ni moja ya njia ya kuziboresha zaidi. Hakuna sababu kuwa na barabara za kisasa na wakati huo abiria wanaosafiri katika barabara hizo wanakosa huduma muhimu kama vyoo na mahali pa kupumzika.

Natoa rai kwa wadau na mashirika mbalimbali nchini kuiga jambo hili jema na kusaidia shughuli hii muhimu. Barabara za nchi yetu ni nyingi na maeneo ni mapana, hivyo kwa taasisi moja peke yake kufanya jambo hili ni kazi ngumu, zinahitajika juhudi za pamoja na ushirikiano mkubwa katika kufanikisha. Mafanikio ya mradi huu yatachangia kwa kiasi kikubwa utunzaji wa mazingira yetu mbali ya kuongeza mapato na kusaidia kupunguza tatizo la ajira. Napenda kutoa wito kwa watumiaji wote wa vituo na vyoo hivyo, kuhakikisha wanavitunza ili viendelee kutoa huduma iliyokusudiwa kwa muda mrefu.

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana;**

Napenda kutumia hadhara hii kuwakumbusha Watanzania wote umuhimu wa kutunza mazingira yetu na kuhifadhi vyanzo vya maji. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kuhakikisha anahifadhi mazingira pale anapoishi kwa kupanda miti na kuepuka vitendo vyote vinavyosababisha uharibifu wa mazingira. Misitu ikipotea tunakosa mvua na matokeo yake ni mabaya kwetu, ndio maana leo hii tunakumbwa na matatizo mbalimbali kama vile kupungua kwa kina cha maji kwenye mabwawa yanayozalisha umeme.

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana;**

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuwakumbusha Watazania wote kwamba Oktoba 25 mwaka huu ni siku muhimu katika historia ya Taifa letu. Tunakwenda kupiga kura ya kuchagua viongozi katika ngazi mbalimbali. Natoa wito kwa Watanzania wote kujitokeza kwa wingi na kutumia haki yao ya kidemokrasia kwa kuchagua viongozi wanaowapenda. Tukumbuke kwamba viongozi tutakaowachagua ndio watakuwa dira ya kuongoza nchi yetu katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Ni imani yangu kwamba mtajitokeza kwa wingi kupiga kura. Napenda kuwahakikishia kwamba sisi katika serikali tumejipanga vizuri kuhakikisha zoezi hilo linamalizika kwa utulivu mkubwa na amani ili tuendelee kudumisha Umoja, na Mshikamano wa nchi yetu.

**Ndugu Wageni Waalikwa;**

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana;**

Kwa kumalizia hotuba yangu, kwa mara nyingine tena napenda kuwashukuru MUET na wadau wote kwa kunialika hapa siku ya leo. Niwashukuru pia wadau mbalimbali waliojitokeza kuunga mkono jitihada hizi za ujenzi wa vituo vya mapumziko na vyoo. Kipekee tunaipongeza Serikali ya China, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kampuni ya simu za mkononi ya Airtel, Ndugu Mustafa Sabodo, Mufindi Tea Company, MUCOBA BANK, PSPF na TANESCO.

Baada ya kusema haya kwa heshima kubwa na taadhima sasa natamka rasmi kwamba; ***Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Mapumziko na Vyoo kwa Wasafiri katika Barabara Kuu nchini, umezinduliwa .***

**Asanteni sana kwa kunisikiliza**